



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA GEITA



**TAARIFA KWA UMMA**

**BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA MANISPAA YA GEITA  
LAPITISHA RASIMU YA BAJETI YA SHILINGI BILIONI 68.3 KWA MWAKA WA  
FEDHA 2025/2026**

Leo tarehe 30 Januari, 2025 Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmshauri ya Manispaa ya Geita umeridhia na kupitisha rasimu ya bajeti ya Shilingi Bilioni **68,393,812,906.00** kwa mwaka wa fedha **2025/2026**. Bajeti hii ina ongezeko la **13.2%** zaidi ya ile ya mwaka wa fedha **2024/2025**.

Kati ya bajeti hiyo shilingi bilioni **47,547,078,004.00** sawa na **69.6%** ni ruzuku kutoka Serikali Kuu na Shilingi bilioni **20,846,734,902.00** sawa na **30.4%** zitatokana na mapato ya ndani ambayo ni ongezeko la **asilimia 4.2** kutoka bajeti ya mwaka **2024/2025** kwa Shilingi bilioni **19,965,455,000.00**

Akiwasilisha rasimu ya bajeti hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mji, Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu Halmashauri ya Manispaa ya Geita, Ndg. Samson Ndaro amesema Halmashauri inakadiria kupokea na kutumia jumla ya shilingi **68,393,812,906.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Ndg. Ndaro ameongezea kusema vyanzo hivyo ni mapato ya ndani shilingi bilioni **20,846,734,902.00**, matumizi mengineyo (Ruzuku ya Serikali) shilingi bilioni **1,031,607,000.00**, Mishahara (Ruzuku ya Serikali) shilingi bilioni **32,286,649,150.00**, miradi: fedha za ndani (Ruzuku) shilingi bilioni **4,219,164,414.00**, miradi: fedha za nje (Wahisani) **4,634,413,000.00**, CSR shilingi bilioni **5,025,244,440.00** na michango ya wananchi na wadau wengine wa maendeleo shilingi milioni **350,000,000.00**

Aidha, Ndg. Ndaro amesema vipaumbele vya bajeti hiyo ni kuongeza mapato ya ndani kutoka bilioni **19,965,455,000.00** ya sasa hadi bilioni **20,846,734,902.00**, ili kuimarisha shughuli za utawala bora, Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya, Uimarishaji wa usafi wa mazingira, Kuboresha miundombinu ya shule za

Msingi, Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Ukamilishaji wa miradi viporo, Umilikishaji wa maeneo ya umma.

Aidha Waheshimiwa Madiwani wameonesha kuwa na Imani na maono chanya katika maandalizi ya mipango na bajeti ya mwaka wa fedha **2025/2026** ikiwemo Baraza la wafanyakazi, kamati ya ukimwi, kamati ya elimu, kamati ya uchumi, ujenzi na mazingira, kamati ya fedha, Utawala na mipango.

Hata hivyo katika Baraza hilo la kupitisha rasimu ya bajeti Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Geita Ndg. Yefred Myenzi amewapongeza Waheshimiwa Madiwani wa kata zote kwa kuwa wafuatiliaji wa miradi ya maendeleo na michango yao katika kuendeleza Halmashauri, Pia ameishukuru Serikali kwa kutoa fedha za kuendeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya maji, barabara, umeme, ujenzi wa shule na vituo vya Afya.

Akizungumza katika mkutano wa Baraza la Madiwani la kujadili na kupitisha rasimu ya bajeti hiyo Januari 30, 2025, Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Geita Mhe. Costantine Morandi Mtani amesema bajeti hiyo imezingatia mapendezo yote muhimu ya waheshimiwa madiwani na hivyo itakwenda kutatua changamoto mbalimbali za wananchi.

Uandaji wa Mpango na rasimu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26, umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu na. 21 cha sheria ya bajeti, sura **439** na kanuni zake za mwaka **2015**. Maandalizi ya mpango huu wa bajeti yamezingatia ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mpango wa tatu wa maendeleo ya Taifa wa miaka mtano 2021/22 - 2025/26, malenzo ya maendeleo endelevu 2030 na maelekezo mahsusi ya serikali.



J. Y. Mbilinyi

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**30 Januari, 2025**